# NANI ANA AMUA?



Elewa ushiriki wa watendaji mbalimbali katika sekta ya madini kutoka uchimbaji wa madini nchini DRC

# KWANINI NI LAZIMA KWAKO KUSOMA HII ?




Madini ya DRC yanatafutwa sana kwa utengenezaji wa simu, kompyuta ao laptop na magari. Imepelekwa kwenyi ma fonderies hambapo madini imegeuzwa kuwa metali. Metali hizi zina matumizi tofauti. Mkusanyiko wa hatua hizi zote ndio **unaitwa ngazi za usambazaji (chaîne d'approvisionnement).**



DRC imejulikana kama fasi yenye hatari kubwa kutokana na fudjo za vita, hasa mashariki (est) ya inchi, pamoja na kukosa kuheshimu haki za binadamu. **Mengi ya mipango hii ilifanyiwa inje ya DRC**. Hata hivyo, inawagusa wafanyakazi na watendaji wengine wote katika madini ya DRC. Kwa sababu hii, ni lazima kuelewa jambo kuhusu chaîne d'approvisionnement ni nini.

# MADINI KUTOKA DRC IKO NA MA FAA KANI?






**Cassiterite ni madini ya bati** (étain) ni ya mafaa kabisa. Inasaidia kufanya kopo, lakini pia kwa wafanyakazi ya byuma yaku fanya soudure.

**Coltan, enye inatosha tantalum na columbium**, inatumikishwa ndani ya telephone, lakini pia katika enjini za ndege.

**Shaba ama cuivre** inatumikishwa katika kazi ya kujenga, transport na sekta ya umeme.

**Cobalt na lithiamu** iko na lazima sana kwa ajili ya kutengeneza piles na baterries rechargeable ao high voltage. Cobalt hutumiwa kwa utengenezaji wa baterries za lithiamu-iyo ni kwa magari ya umeme.

# USAMBAZAJI HALALI (APPROVIONNEMENT RESPONSABLE)

Ma kampuni ya uchimbaji wa madini ambayo yanatoka DRC lazima wabebe responsabilités ya mambo mbalimbali kutokeya na makazi yao na waweze pia kuleta suluwisho (solution).

**Hii inaitwa shurti za uangalifu (devoir de diligence).** Kampuni zinaitwa kupanda kwenye maeneo ya uchimbaji na kuhakikisha ya kwamba hakuna ukiukwaji ya kanuni za kazi wakati wauchimbaji wa madini hayo.

Katika Shirikisho ama Muungano wa Ulaya (Union Européenne), sheria ya 2021 ina shurtisha ma kampuni kufanya uangalizi wa sheria ya binadamu (droits humains) na ya mazingira kuhusu madini kutoka maeneo yaliyoguswa na vita kama vile DRC.

**Neno usambazaji halali (approvisionnement responsable)** inaamanisha kwamba mununuzi anauza na ufahamu (conscience) na uangalifu kutoka kwa chanzo cha maadili (ethique) ambacho huepuka hatari kama vile ukiukwaji wa haki za binadamu (violation des droits de la personne), kukata midomo, ma accidents yenyekuleta vifo, wa mama wa mimba na kazi za watoto ndani ya maeneo ya Madini.

**Usawanyishaji kiserikali (formalisation)** inaomba kupata permis ao kibali ya uchimbaji wa madini kwa mikono na machine ndogo ndogo. Kanuni ya Madini ya Congo ama code minier ya Congo, inaruhusu ma coopératives ya ushirika ya uchimbaji madini kufanya kazi katika kanda za uchimbaji madini ao Zones



# KUFATILIA NA MIPANGO YA KUDHIBITI AO CONTROLE

Concept ya kufatiliya nikutambua na kufuatilia fasi ile madini inatoka pamoja vilevile na matumizi yake. Hii inahusika kufuatilia madini kutoka fasi ya uchimbaji mpaka fasi ya kuuzisha. Hatua hizi zinaambatana na teknolojia inaomba wasambazaji ama fournisseurs kwamba wanashiriki ama kugawanya ripoti ya kila siku kuhusu kwenye madini hayo imetokeya, ilikuhakikisha ya kwamba hakuna ukiukwaji wa Haki za binadamu, uharibifu wa mazingira ao matatizo ndani ya jamii.

Mlolongo wa ulinzi unahusisha kurekodi mfuatano wa watu au taasisi zinazosimamia madini wakati wanapitia mnyororo wa usambazaji



# UTAMBULISHAJI (CERTIFICATION) NA UWAZI (TRANSPARENCE)



**Certification** ni uthibitishaji ama verification ya madini ao namna kwa ajili ya kuhakikisha kwamba zina heshimu kanuni mbalimabli. Mpango wa kwanza wa utambulishaji ulikuwa mpango unaoitwa "processus ya Kimberley" ambayo ina husika na alimasi (diamants).

**Uwazi** inaonesha vile habari inapatikana kwa urahisi ao kwa uteketeke. Bila hivyo, wanunuzi hawawezi kutambua wasambazaji na ngazi zao za usambazaji.

# MADINI YA VITA

Kulingana na NGOs za kimataifa, vita ao fudjo ya masasi inchini DRC inatokana na hamu ya makundi yenye masasi juu ya kufatiliya fasi kunakuwa madini ya inchi na kuweza kuendelesha vita.

Mwaka 2010, Sheria ya Madini ya vita ya Dodd-Frank ya Marekani ililenga bati, tantalum, tungsten na zahabu kutoka DRC. Sheria hiyo, ambayo mara nyingi imeitwa "sheria ya Obama" **ililazimisha ma kampuni kuhepuka kutumikisha n'a kuuza "madini ya vita" yoyote kutoka DRC na inchi jirani.** Sheria kama hiyo ipo katika Union Européene.



# HATARI ZA HATUA ZA KUMALIZA "MADINI YA VITA" NCHINI DRC

Hatari mbaya zina jionesha kwa vituo vya biashara, wafanya biashara, ma fonderies ya ndani na hata washikamaji wote ambayo wana wasilihana, lakini zaidi ya yote pia kwa wanaume na wana wake wanaofanya kazi za madini, wenyeji wa mashimo na wale wanaonyangula mizigo.

**Machambuzi mbaya** (critiques) nyingi zimefanywa ju ya hatua za kukomesha "madini ya vita":

- Garama kubwa ama cout élevé na faida ndogo kwa wachimbaji wadogo katika mahali ambazo zimeguswa na vita (régions touchées).
- Uwezekano wa kupiga marufuko kutokana na chaine d'approvionnement.
- Hatari mbaya za kijamii na kiuchumizi hatua hizi kwenyi terrain.
- Hatari za programu kwenye soko, ambazo ni maendeleo ya wachuruzi wakubwa ambao wanazuwiya wachimbaji wadogo.
- Kukosa kusikiya na kuitikiya wasiwasi ya wa Kongomani.



# NA HATARI KATIKA DRC?

Katika miaka zilizopita, **madini ya DRC yamekuwa lengo ama cible ya programu kubwa kwa ajili ya kusaidia wanunuzi kuheshimu sheria.**

Hatuwa hizi zina angaliya zaidi :

- 3TG (bati, tantalum, tungsten na zahabu) kutoka Kivu Kaskazini na Kivu Kusini, majimbo mawili yaliyo guswa na vita.
- 2C (shaba na kobalti) kutoka Haut-Katanga na Lualaba, zilizotafutwa sana tangu 2017.

Kwa mfano, tunaweza kutaja miradi kuhusu :

- Kukataza kuwepo kwa watendaji wenye silaha ndani ya mine.
- Kuwaondoa watoto ndani ya mines naku wapeleka shule.
- Kutafuta kukataza wa mama wa mimba kuingiya ndani ya mine.



# NA USHIRIKI WA WACHIMBAJI WADOGO?



Jamii zilizoguswa mara nyingi haziwezi kutegemea wakubwa waliochaguliwa kutowa kanuni na shurti kuhusu ngazi za usambazaji (chaines d'approvisionnement) kwa jina yao. Wanazidi "kusimamiwa" nawatendaji wakigeni mara nyingi.


Mipango ya kimataifa ya washikamaji mbalimbali inakazisha ma structures ya mamlaka kwa kutanguliza faida za ma kampuni kuliko yale ya wanainchi. **Hawaingize wachimbaji wadogo kwenye mkusanyo wakati wa kubeba decision.**

Wachimbaji wadogo wanalalamika kuhusu ukosefu wa fasi iliyofaa wakuchimba madini (ZEA) na usaidizi kwa wachimbaji wadogo na jamii, vilevile sauti zao kwa kiasi kikubwa hazi kusikilizwa ndani ya EMAPE.

Ingawa inatambulika kuwa wanawake wapo katika EMAPE, bado wanakabiliwa na kutengwa. Hawaruhusiwi kufanya kazi katika visima vya chini, mahali kuna kuwa kazi zinazo lipwa vizuri zaidi.

Katika fasi yamaeneo ya uchimbaji madini, imekatazi wa kwa wanawake kuwa kwenyi Enzo za madini, lakini kulingana na sheria ya Kongo, ni wanawake wa mimba pekee hawa ruhusiwi.

# MIPANGO YA LAZIMA NCHINI DRC: ITSCI



Mpango wa chaine d'approvisionnement uitwao Tin Supply Chain Initiative (ITSCI), mpango wa uangalifu katika sekta ya bati, tantalum na tungsten, ulianziwa mashariki ya DRC mwaka wa 2010 na chama cha biashara ya bati duniani.

Lengo ama objectif ni kuweka chaine d'approvisionnement ya madini ambayo hailingane na fudjo ao vita ya silaha ao kukosa kueshimu haki za binadamu. Mwaka wa 2011, Tantalum-Niobium International Study Center (T.I.C.), ambayo ina shimamiya tantalum na niobium, ilijiunga na usimamizi wa ITSCI.

**Katika mines ambapo ITSCI inafanya kazi, kuna namna ya kuweka étiquette kwa mikono kwa ajili ya kufuatilia safari ya madini kutoka fasi za uchimbaji zilizo julikana chini ya etiquette** (pia inajulikana kama tag) hadi kwenye fonderie. Maeneo ya uchimbaji madini yana fuatiliwa na watumishi wa ITSCI kwa ushirikiano na serikali ya DRC, hasa SAEMAPE (Huduma ya Usaidizi na Usimamizi wa uchimbaji madini kwa mikono na Migodi ndogo ndogo). ITSCI ina pewa pesa ambazo wasafirishaji wanalipa.

Ripoti ya shirika lisilo la kiserikali la kimataifa la Global Witness (2022) iliweza **kusema kuwa ITSCI ilipatikana katika utoroshaji wa "madini ya vita" na kwamba madini mengi yenye étiquettes yalitoka kwenye mines ambayo haikuwa inspecter.**

# UCHIMBAJI BORA

Uchimbaji Bora ni mpango wa ufuatiliaji katika sekta za 3T na 2C kwa objectif la kuendelesha hali katika maeneo ya EMAPE. Uchimbaji Bora wa Madini husaidia ma kampuni kupata kwa namna zilizo itikiwa kuwa halali kwa kutoa uzibitisho wa chaine d'approvisionnement kwa kutumia alama 16 za uangalifu, ambazo zina lingana na Guide ya Muungano wakimataifa unao julikana kwa jina ya OCDE juu ya uangalifu unaostahili kwa maeneo katika vita ao maeneo ya hatari kuu.

Uchimbaji Bora pia inatafuta kuwezesha makampuni kusaidia maendeleo ya maeneo ya EMAPE na jamii zote jirani.

Kama vile ITSCI, **Uchimbaji Bora huweka étquettes kwenye mifuko na kuzifuatiliya hadi mahali zinapo uzwa inje**. Uchimbaji Bora hutengeneza mipango ya kuepusha (PAC) na wasimamizi wamaeneo za uchimbaji madini ili kukabiliana na "hatari" zilizo tambuliwa.



# Muungano wa Haki Cobalt (FCA)

The Fair Cobalt Alliance (Alliance du cobalt équitable) ni plateforme ya wafanya kazi mbalimbali lililo anziwa mwaka wa 2020 na The Impact Facility (TIF), shirika linalo ongozwa na biashara inchini Uwingereza (Angleterre).

Lengo ya FCA ni **kuongeza usambazaji wa cobalt ya ufundi inayo kubaliwa na ma kampuni, kwa kufuata makanuni ao normes ya kimataifa**. Shirika inataka kuendelesha hali katika maeneo ya uchimbaji madini nakusaidia maendeleo ya jamii.

Maono ya FCA ni pamoja na :

- Kuendelesha afya na usalama kazini.
- Mazingira mazuri yakufanya kazi.
- Kupunguza kutumika kwa watoto.
- Kuongeza pato (revenus ya watu).

FCA ina wanachama 24 piya na mashirika indutriel na biashara (RCI na Taasisiya Cobalt), ma kampuni ya uchimbaji madini kama vile Glencore na CMOC na mashirika yasiyo ya faida.

Moja ya projet iliyo anzishwa na FCA inatekelezwa kwa ushirikiano na chama cha ushirika cha CMDS kilipo kuwa Kamilombe ikiwa ni pamoja na utoaji wa vifaa vya kujikinga binafsi kwa waoshaji wanawake wa Kamilombe.



# KUFATILIA : ufuatiliaji na taarifa za matukio

Mtu yeyote anaweza kuripoti tukio kwenye jukwa hili la SMS na WhatsApp, ambalo ni bure, na jina alitaoneshwa na pia ni bure. Système inaundwa kwa kiotomatiki horodha ya matumizi kuhusu incident, ambayo mtumiaji anaweza kujibu bila kujulikana kwa Kiswahili, Lingala, Kifaransa ao Kingereza.

Kufuatia mwongozo wa OCDE, Kufatilia ina kamata aina saba za incidents: "ajali za ndani ya mines, mvurugo, kutumika kwa watoto, kukata milomo/udanganyifu, vizuizi vya barabarani, tatizo la mazingira, migogoro na kampuni ya viwanda, na bingine".

Ma OSC inapashwa kuonesha ma incidents na wa acteur waliofaa, ikiwa ni pamoja na mamlaka za mitaa, polisi, vituo vya uchimbaji madini za serikali, vyama vya ushirika vya uchimbaji madini, jeshi na/ao societé civile locale.

Kufatilia ni projet yenyi kuripoti na **ufuatiliaji wa ma incidents ili kuwezesha kuripoti na ku fatiliya ndani ya uwasiliano pamoja na mashirika za kiraiya** (OSC). Carte web ku mutandao (internet) ina kuruhusu kutazama ripoti za matukio kwa wakati wa kweli. Projet iyi inatumika Kivu Kusini, Kivu Kaskazini, Ituri; Haut-Uélé na Lualaba.



# MFUMO WA UDHIBITI WA DRC

Katika mwaka wa 2010, serikali ilianza ku cartographier ma sites zisizo julikana kiserikali (informels) ndani ya EMAPE na kuzitafautisha kulingana na kama zilikutana na utaratibu wa certification kutokeya Mkutano wa Kimataifa wa Ukanda wa Maziwa Makuu (CIRGL). Maeneo hayo yamethibitishwa kuwa yakijani, njano, nyekundu ao bluu.


Katika mwaka wa 2018, Kanuni mpya za madhini ambazo ilichukuliwa, zinaishimu kanuni za kanda ya majimbo na kimataifa kuhusu certification.

Kulingana na Kanuni za Madini, gavana ama gouverneur wajimbo anakuwa responsable wa kujenga vituo vipya vya kuuzisha. Huko Kolwezi, kwa mfano, kituo cha biashara cha Musompo kilifunguliwa mwaka wa 2020.

Mwaka 2021, DRC ilianza Entreprise Générale du Cobalt (EGC) kama mnunuzi mpya wa cobalt ya ufundi, kwa kufuata ma shurti ya usambazaji iliyo faa. EGC itakuwa muigizaji pekee anaweza kuuza, ku traiter na kuuzisha kobalti ya ufundi kutoka DRC. Itaweza kupunguza usafirishaji usio julikana (transport illegal) wa kobalti na kukabiliana na hali mbaya ya kazi ya wachimbaji wadogo.

Mashariki mwa DRC, jimbo la Kongo limeunda Kampuni Hodhi, Primera Gold DRC SA, kwa lengo la kuunda mnyororo wa ugavi wa dhahabu "bila migogoro". Kampuni hii ina Bodi ya Wakurugenzi mchanganyiko: DRC na Umoja wa Falme za Kiarabu. Inasimamia kituo cha ununuzi wa dhahabu, uuzaji na usafirishaji wa nje.








Besoin kubwa ya kusikiliza zaidi wachimbaji wadogo kwa mikono. Moja wapo ya malalamiko ya wachimbaji wa madini ni kuhusu beyi ya madini, tija (ongezeko ya utowaji madini) na haki ya kutumika huru na bila fukuzwa ndani ya maeneo ya uchimbaji.

iki weza zaidi Ku fwatana na ugavi pamoja na uzalishaji duniani. Kawaida, beyi uangalifu ni hizo za LME (London Métal Exchange, www.lme.com)na kuhusu zahabu ni kwenyi London Bullion Market Authority (LBMA, htpps://www.lbma.org.uk/). Lakini, kuna kuwa tafauti kati ya beyi kwenyi soko za kimataifa na beyi inchini RDC. Nyumbani ama mjini, beyi ina ambatana vilevile na samani (teneur) pamoja na uwingi (quantité) wa madini (vilevile kupata vyombo kemkemu kwaajili ya kupima hiyo) na hata mara moja moja, mapatano za wanunuzi na wachuruzi.

Utungo kibuni: Sarah Katz-Lavigne na Sara Geenen

Picha: Mélissa Jina, Ampreinte na Belushi studio

Tafsiri ya maandishi: Espérant Mwishamali na Philippe Dunia

Utungaji: Gabriel Muhanzi

University of Antwerp IOB Institute of Development Policy

CEGEMI centre d'expertise en gestion minière

vliruos SHARING MINDS, CHANGING LIVES

fwo Research Foundation Flanders Opening new horizons

Kutosha wa fadhili ambao wametajwa juu, atukupata musaada wa fedha yoyote.